SautiElimu

hakielimu

Toleo la 4
2003

ISSN 0856 8588

HakiElimu • Mtaa wa Mathuradas Na 739 • SLP 79401 • Dar es Salaam • Tanzania • Simu (255 22) 2151852 au 3 • Fax: (255 22) 2152449 • Barua Pepe: info@hakielimu.org • Tovuti: www.hakielimu.org

Usitilie Shaka Uwezo Wako wa Kuleta Mabadiliko

Na Rakesh Rajani, Mhariri Mkuu

Mara kwa mara huwa nakutana na watu wanaopenda kusema: “mimi mtu maskini siwezi kufanya kitu” au “sisi wanyonge hatuna uwezo wa kuleta mabadiliko” au “tunaomba pesa na kujengewa uwezo ili tupate maendeleo”.

Kwa kweli baada ya muda unyonge huu unaanza kuchusha!

Ni kweli kuwa tajiri au kiongozi anaweza kufanya mambo yake kwa urahisi zaidi. Ni kweli kuwa ni vigumu kwa waliofukarishwa au kubaguliwa katika kupata fursa ya kujiendeleza kufikisha malengo yao. Lakini, bado kila mmoja ana uwezo! Kila mmoja ana mawazo, fikra, hisia, ari na nia. Kwa kushirikiana na wenzetu, sisi sote tunaweza kuboresha elimu, kuchangia kuleta usawa na haki, na kujiendeleza.

Mwandishi maarufu wa Marekani, Margaret Mead, aliwahi kutamka “Never doubt that a small group of thoughtful, committed citizens can change the world; indeed, it’s the only thing that ever has”; akiwa na maana kwamba tusiwe na shaka kwamba kikundi kidogo cha wananchi wenye fikra, wenye kujituma kinaweza kugeuza dunia.

Harakati za Marafiki wa Elimu zinamaanisha kwamba watu wa kawaida wanaweza kuungana, kupashana habari, kujifunza, kupanga na kutenda kwa ajili ya kuleta mabadiliko. Toleo hili linaelezea madhumuni ya *Harakati za Marafiki wa Elimu*, linaarifu kuhusu shughuli za baadhi ya Marafiki wa kwanza, linatoa maoni ya *Marafiki* juu ya elimu na linakualika kujiunga.

Usitilie shaka uwezo wako wa kuleta mabadiliko!



Harakati za *Marafiki* Kuboresha Elimu Zaanza Mwanza

Na Godfrey Telli

Harakati za Marafiki wa Elimu zimeanza kupamba moto sehemu mbalimbali. Wanaharakati 34 wa Isamilo Mtaa wa Benki Kuu jijini Mwanza walijadili kwa kina kuhusu elimu waipatayo watoto wao shuleni.


Walijadili suala la wazazi kujali na kufuatilia habari za elimu ya watoto wao. Walitafakari juu ya sauti ya wanyonge kusikika katika elimu. Wakajiuliza; je wanapokwenda katika ofisi za serikali kuulizia masuala ya elimu wanapokelewa na kusikilizwa? Wakagundua upungufu mkubwa katika eneo hilo, hasa katika masuala yanayohusu matumizi ya fedha na masomo ya ziada ya wanafunzi wakati wa likizo. Wameona kwamba kwa wazazi masikini elimu ya watoto wao inashuka na kuwa duni zaidi kwa kukosa fedha za masomo ya ziada (tuition).

Katika kikao hicho wajumbe pia walijiuliza kama wanafahamu jinsi fedha za shule yao zinavyotumika. Wengi walieleza kwamba suala hilo hawalifahamu vyema kwa sababu kila wanapodadisi kuhusu mapato na matumizi ya fedha shuleni, walimu wanakuwa wakali. Waliazimia kuzidi kulifuatilia jambo hilo kwa msaada wa Mkuu wa Mkoa wa Mwanza.

Mjadala uliendelea kuchambua masuala ya michezo kwa wanafunzi, umuhimu wake na maendeleo ya taaluma ya watoto kwa kufuatilia kila mara wanachojifunza shuleni. Pia waliangalia adhabu za viboko zinavyotolewa shuleni bila sababu za kimsingi. Kwa mfano mtoto anaadhibiwa kwa ajili ya kudadisi utata wa alama za kufaulu mitihani zinapotofautiana kwenye ripoti na kwenye karatasi ya mtihani.

Huu ni mfano bora wa *Marafiki wa Elimu* walioamua kuanza kuleta mabadiliko kwenye jumuiya yao!

Na wewe je?



Wananchi Wataletaje Mabadiliko ya Sera?

Na Marjorie Mbilinyi

Harakati za Marafiki wa Elimu ni nafasi kwa jamii kuchangia maoni yao juu ya elimu na demokrasia. *Marafiki* ni washiriki kutoka vikundi mbalimbali vya kijamii wakiwemo walimu, wanafunzi, watoto na vijana wasio wanafunzi, wazazi, viongozi wa serikali za mitaa na vikundi au taasisi za kijamii.

Harakati za Marafiki wa Elimu zinaraghabisha mikakati ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM) na sera zinazolenga kuboresha elimu chini. Zinatoa nafasi kwa wananchi kuchangia juu ya utekelezaji wa sera kwa kuchambua na kuainisha zile zilizo bora na zile zenye upungufu katika utekelezaji wake. Kwa mfano, sera ya kuboresha serikali za mitaa kwa kurejesha mamlaka na rasilimali kutoka serikali kuu kwenda kwa wananchi.

Mkakati wa Kupunguza Umaskini unatoa viashiria vya kupima mafanikio kutoka katika jamii. Serikali inatakiwa kutathmini mafanikio yake na kujua kama rasilimali zinawafikia wananchi kwa kupitia viashiria hivyo. Inahitaji mrejesho kutoka kwa wananchi katika mchakato wa kutathmini. Kwa hiyo maoni ya *Marafiki wa Elimu* ni muhimu. Kuchangia maoni na kufanya majadiliano ni jambo lilo bora. Lakini je, inatosha tu kuchangia maoni? Wanajamii wanaweza kujenga nguvu za pamoja kama vile vikundi vya hiari vya kiraia. Lakini je na hiyo inatosha?

Habari zinazotoka kwa wanajamii, majadiliano yao na nguvu zao za pamoja za kutoa msukumo zinahitaji kufikishwa kwa watunga sera pamoja na umma. Hapa ndipo jukumu letu HakiElimu linapoingia. Tunawasikilizaje? Tunanukuu vipi maoni yao? Tunayafikishaje maoni yao huko juu? Tunapaswa kusambaza maoni na habari zao. Lakini hapa napo je inatosha?

Hayo yote hayatoshi. Wananchi wanaongea sana, wanachambua sera na kutoa maoni yao ambayo yanapaswa yasikilizwe na waunda sera, serikali, wafadhili, n.k. Maoni yao yakisikilizwa, yakisambazwa na yakifika kwa wanaohusika, yanafanyiwa kazi? Mabadiliko gani makubwa yametokana na shughuli zao? Tufanyeje kuhakikisha kwamba mfumo wa jamii unabadilika kufuatana na rai ya wananchi? Hiyo ndiyo changamoto iliyoko mbele yetu sisi sote.



Je, Wajua Kwamba *Marafiki wa Elimu*....

Na Godfrey Telli

- ni harakati za watu wanaojali, mashirika na taasisi zenye nia ya kuboresha na kuleta mabadiliko katika elimu nchini?
- hutoa fursa kubwa zaidi kwa watu wanaojali elimu Tanzania kushirikiana na wenzao? Kufanya mijadala na kutoa maoni yao kuhusu kuboresha elimu nchini na kuleta mabadiliko katika jamii? Hii ina maana kwamba ni wewe utakayeanza kuleta mabadiliko!
- hutoa fursa kwa kila mmoja wetu kuweza kujiunga? Hakuna vikwazo; uwe kijana au mzee, mwanamme au mwanamke, uwe shuleni au nje ya shule. Pia hakuna gharama yoyote ya kujiunga.
- hutoa fursa ya kutoa maoni na kero zako kwa viongozi husika wa elimu na kubadilishana mawazo na watu wenye fikra na maoni mbalimbali kuhusu elimu na utawala bora?
- hutoa fursa ya kupata machapisho yenye taarifa za mara kwa mara kuhusu sera ya elimu, utawala bora na shughuli za *Marafiki wa Elimu* kutoka sehemu mbalimbali?
- wana jukumu la kuongoza harakati hizi na kuleta mabadiliko ya elimu? Kuimarika kwa harakati hizi kunakutegemea wewe, na kwamba HakiElimu ni mraghabishaji tu wa harakati hizi?
- wameanza kuchukua kasi? Watu wengi wanazidi kujiunga? Mijadala motomoto imeanza kufanyika kila kona ya nchi yetu? Vikundi vya wanaharakati vimeanzishwa?

Na wewe usisubiri! Jiunge sasa! Anzisha mijadala! Leta mabadiliko!

Kujiunga na *Harakati za Marafiki wa Elimu* ni rahisi! Tuandikie aya moja kueleza nia yako ya kujiunga, umri, jinsi, anuani ya Posta, Simu, Fax, Barua pepe na saini yako.

Anuani yetu ni: *Marafiki wa Elimu*
C/o HakiElimu
SLP 79401
Dar es Salaam
Tanzania
Barua pepe: rafiki@hakielimu.org
Tovuti: www.hakielimu.org

Marafiki wa Elimu watafanyakazi kwa niaba yao na kufuata sheria za Tanzania na mikataba ya kimataifa iliyopitishwa na nchi. Wakati wowote, *Marafiki wa Elimu* hawatafanya kazi kwa niaba ya HakiElimu wala washirika wake. *Marafiki wa Elimu* watawajibika kwa matendo yao wenyewe. HakiElimu na washirika wake hawatawajibika wakati wowote kutokana na matendo ya *Marafiki wa Elimu.*

Ukurasa wa 1

SautiElimu

hakielimu

Toleo la 4
2003

ISSN 0856 8588

HakiElimu • Mtaa wa Mathuradas Na 739 • SLP 79401 • Dar es Salaam • Tanzania • Simu (255 22) 2151852 au 3 • Fax: (255 22) 2152449 • Barua Pepe: info@hakielimu.org • Tovuti: www.hakielimu.org

Utoro Unasababishwa na Nini?

Utoro wa wanafunzi shuleni umekuwa moja ya matatizo makubwa hapa nchini. Tatizo hilo linasababishwa na mambo mbalimbali. Baadhi ya wanafunzi wa Shule ya Msingi ya Halwego wilayani Ukerewe wamepata nafasi ya kutoa maoni yao kuhusu sababu za utoro shuleni.

Paschazia Victor (12) wa darasa la sita anasema watoto wengi hukosa kwenda shuleni kwa sababu wazazi huwalazimisha waende shambani hata kwa wiki nzima bila kupeleka taarifa kwa walimu. Kwa kufanya hivyo watoto hukosa masomo na hivyo matokeo yake hata kwenye mitihani yao hufanya vibaya. Kutofanya vizuri kwenye mitihani nako husababisha mwanafunzi kuwa mtoro. Paschazia anatoa ujumbe kwa wazazi wasiwazuie watoto wao kwenda shuleni.

Naye Adventina Maunda (16) wa darasa la saba anasema utoro unasababishwa na wazazi kutofuatilia watoto wao wanapotoka shule. Mtoto huvaa vizuri nguo kama anakwenda shuleni kumbe akifika huko anakwenda porini kuwinda; muda wa kurudi nyumbani ukifika naye anarudi. Wazazi hawamwulizi kama amesoma au la. Sababu nyingine ni walimu kuwa wakali. Baadhi ya walimu wanapiga bila huruma kiasi kwamba mtoto akimwona mwalimu anajificha hadi saa ya kurudi nyumbani. Anatoa wito kwa walimu kupunguza ukali kwa wanafunzi ili wasiwaogope.

Mabusi Ferdinandi (15) wa darasa la nne anasema sababu za utoro shuleni ni kukosa sare za shule na walimu kupiga bila huruma. Anaendelea kusema kuwa wazazi nao huchangia watoto wao kutoroka kwani watoto wakiwaambia wawanunulie sare za shule husema, “Nenda tu wakikufukuza basi!” Mabusi anawaomba walimu kuacha kupiga wanafunzi na wazazi kuwanunulia watoto wao sare za shule.



Maoni ya Rafiki Kuhusu Elimu


Na Jumanne Isike, Kakola- Tabora

Mimi ni *Rafiki wa Elimu* kutoka Tabora. Ninafurahishwa sana na *Harakati za Marafiki wa Elimu* kujali na kutetea haki za kila mtoto kupata elimu bora. Ninaamini kwamba huu ni mwamko kwa kila mwanajamii.

Lakini kuna jambo moja linalonihuzunisha sana. Jambo hilo ni ajira mbaya kwa watoto. Je, mnafahamu kwamba watoto wadogo walioajiriwa hawapati muda wa kwenda shule kusoma na pia hawapati muda wa kucheza na watoto wenzao?

Sababu hiyo imenifanya niamue kupambana na ajira mbaya kwa watoto kwa vitendo. Ninawakaribisha *Marafiki wa Elimu* wengine kujiunga nami katika vita hii. Mimi ni mwanachama wa shirika moja linalotetea haki za watoto kupata elimu na kupambana na ajira mbaya kwa watoto.

Niko tayari kuwaunganisheni katika shirika hilo ili tufanye kazi kwa pamoja na kuhamasisha upatikanaji wa elimu bora kwa watoto wote nchini!



HakiElimu ni Shirika la hiari linalolenga kufikia usawa, ubora, haki za binadamu na demokrasia katika elimu kwa kuwezesha jamii kubadili shule na mfumo wa uundaji sera za elimu, kuimarisha ubunifu wa uendeshaji wa mijadala na midahalo ya umma, kufanya utafiti yakinifu, wenye kuhoji, kuchambua, kutetea na kushirikisha wadau ili kuendeleza manufaa ya pamoja na kuzingatia haki za jamii.

Unaruhusiwa kunakili sehemu yoyote ya kijitabu hiki kwa minajili isiyo ya kibiashara. Unachotakiwa kufanya ni kunukuu chanzo cha sehemu iliyonakiliwa na kutuma nakala kwa HakiElimu.

ISSN 08568588
© HakiElimu, 2003
Mhariri Mkuu: Rakesh Rajani

Timu ya *SautiElimu*: Mary Nsemwa, Lilian R. Kallaghe, Godfrey Telli na Connie Francis.
Mchoraji: Marco Tibasima

Tuandikie!

HakiElimu, *SautiElimu*
SLP 79401
Dar es Salaam
Simu: 022 2151852 / 3
Faksi: 022 2152449
Baruapepe: info@hakielimu.org
Tovuti: www.hakielimu.org

Barua kwa SautiElimu

Kwako Mhariri,
Mimi ni mwanaharakati namba 176. Napenda kufungua mjadala na kutoa changamoto kwa wanaharakati wa *Marafiki wa Elimu* juu ya haki za watoto.



Moja ya kifungu katika Mkataba wa Haki za Watoto kinasema kuwa elimu anayopata mtoto imfundishe kuheshimu haki na uhuru wa watu wote. Je, tunawezaje kutekeleza kifungu hicho huku kukiwa na nidhamu ya viboko shuleni? Je bila kuheshimu haki ya mtoto, atajifunzaje kuheshimu haki za wengine?

Ramadhani Lubata
SLP 6808
Dar es Salaam

•••

Kwako Mhariri,
Katika jamii yoyote mwalimu ndiye daraja la kurithisha mila, desturi na utamaduni wa jamii husika kwa vizazi vijavyo. Mwalimu ndiye mjenzi wa awali wa taifa. Kutokana na umuhimu huo, ni vyema mwalimu akaandaliwa mazingira yatakayomwezesha kufanya kazi yake kulingana na mabadiliko yanayoendelea kutokea katika jamii.

Walimu wetu walio wengi hapa nchini hasa wale walioko vijijini hawapati fursa ya kutosha kujifunza na kuyafahamu mabadiliko yanayojitokeza katika utendaji kazi wao wa kila siku. Wengi bado wanatumia nyenzo, ujuzi na mbinu za kizamani walizojifunza wakiwa chuoni ambazo kwa sasa zimepitwa na wakati.

Ili kuboresha elimu nashauri kwa upande wa walimu wajenge tabia ya kujisomea binafsi badala ya kukaa tu na kusubiri nafasi za kujiendeleza kimasomo. Kwa upande wa serikali ningeshauri yafuatayo:

- Uwepo utaratibu endelevu wa kuwapatia mafunzo kazini walimu wote wenye muda mrefu kazini.
- Walimu washiriki katika kuandaa mitaala mipya ili kurahisisha utekelezaji wake.
- Walimu wapewe fursa ya kujiunga na kozi nyingine ambazo maarifa yake yanahitajika katika ufundishaji, mathalan kozi ya ufundi, ushauri nasaha, nk.

Naamini kwamba mchango wa maoni yangu utasaidia katika jitihada za watanzania kuboresha elimu.

Patrick F. Malando
SLP 993
Dodoma

•••

Kwako Mhariri,
Nawapongeza wote waliotoa maoni yao kwenye jarida la *SautiElimu*, toleo la pili. Sisi walimu tuna mzigo mkubwa wa kurundikiwa vipindi vingi kupita kiasi. Mfano katika shule yetu kuna walimu watatu tu kwa darasa la kwanza hadi la saba. Je, elimu bora itapatikanaje shuleni hapa?

Kwa hali hiyo napendekeza kwanza, uwepo mfumo kama unaotumiwa na walimu wa vyuoni. Mwalimu asomee masomo mawili tu na ayafundishe hayo hayo kwa undani. Pili, uwepo muda wa kutosha wa mafunzo kazini kwa walimu ili kuimarisha uwezo wa kufundisha masomo mapya kama vile stadi za kazi. Vilevile ziwepo kozi fupi za mara kwa mara ili kuwawezesha walimu kwenda na wakati. Hayo yote yatawezekana iwapo walimu watashiriki kikamilifu katika kupanga na kutekeleza.

Abel Tollage
Shule ya Msingi Igelango
SLP 74 Ilembula,
Njombe

Kwako Mhariri,
Napenda kuwapongeza waraghabishi wa *Harakati za Marafiki wa Elimu* kwa kazi kubwa mnayofanya ya kutupasha habari na kutuunganisha na wanaharakati wengine wa elimu nchini.

Nawapongeza pia kwa machapisho ambayo yameandikwa kwa lugha nyepesi inayotuwezesha hata watu wenye elimu ya darasa la saba kuelewa sera na masuala muhimu ya elimu nchini. Mfano mzuri ni kipeperushi cha *Marafiki wa Elimu* ambacho kinatuwezesha kuelewa na kwenda na wakati katika ulimwengu huu wa wasomi.

Hongereni!

Mrisho Francis
Kata ya Ipole
SLP 33 Sikonge
Tabora

•••

Kwako Mhariri
Napenda kutoa maoni yangu kwa *Marafiki wa Elimu* nchini kwamba ili kuboresha elimu ni vyema jamii inayoizunguka shule, walimu, wanafunzi, wazazi na viongozi washirikiane kwa kuchambua maeneo yanayokusudia kuimarisha shule.

Vilevile kuwepo na ziara za *Marafiki wa Elimu* wa sehemu moja kwenda sehemu nyingine kuangalia na kujifunza kutoka kwa wengine kuhusu namna ya kuboresha elimu. Kwa upande wa ubunifu kwa wanafunzi, kuwepo na mashindano kupitia michezo mbalimbali, mashindano ya mavazi yaliyobuniwa na wanafunzi wenyewe na usafi wa mazingira.

Kwa walimu, ifanyike tathmini ya mara kwa mara ya ufundishaji kwa kila somo. Napendekeza pia walimu wasikae katika shule moja kwa muda mrefu.

Elias Ngumbilo
SLP 5280
Morogoro

•••

Kwako Mhariri,
Mwalimu ninapompiga mwanafunzi najisikia yafuatayo: (a) Sipendi kumpiga wala sipati faida yoyote, isipokuwa inabidi nimrudi mtoto afuate sheria ya shule (b) Unaweza kutoa adhabu nyingine kama kuchimba visiki, kuruka kichura n.k. sasa je, utatoa adhabu hiyo saa ngapi wakati mtoto amefanya kosa hilo wakati unafundisha? Dakika ni 40 tu na watoto ni 120. Nikitoka hapo nasubiri darasa lingine, kwa siku nina vipindi saba! Hapo sijasahihisha kazi za wanafunzi. (c) Hiyo adhabu nitapata muda upi wa kusimamia?

Makosa kama hayo yanatokea kila darasa; hata ukisema baada ya vipindi huoni kama utapigisha magoti robo tatu ya shule? Hata hivyo si wewe tu uliyekosewa, yupo na mwalimu mwingine. Hata kama una uwezo wa kudhibiti darasa kweli utaweza kwa mazingira hayo? Ili kupunguza matatizo kama hayo ndiyo maana naweza kumfinya au kumchapa kiboko ili nimalize tatizo la kusumbuka tena kufuatilia watu wa adhabu. Ninakuwa nimerahisisha kazi.

Walimu na wanafunzi wanaweza kuheshimiana zaidi iwapo: (a) Mwalimu atakuwa mkali kiasi, asiwe mkali mpaka mwanafunzi amwogope, (b) Mwalimu atamheshimu mwanafunzi na mwanafunzi atamheshimu walimu, (c) Mwalimu atasikiliza matatizo ya mwanafunzi, (d) Mwalimu atajiheshimu yeye mwenyewe.

Mwl. Merian Simon Masangya
Kimpunda Shule ya Msingi
SLP 77 Kiomboi
Singida





Tunapokea maoni kuhusu kuboresha jarida letu.
Pia tungependa kufahamu jinsi wewe msomaji unavyolitumia jarida hili.
Tutumie maoni yako! Ikiwa tutayatumia maoni hayo katika machapisho yetu tutakuzawadia fulana ya HakiElimu.

Ukurasa wa 2